



**Allegheny County Emergency Rental Assistance
(Usaidizi wa Upangishaji wa Dharura wa Allegheny County)
unapatikana ikiwa umepoteza kazi yako au kipato kwa sababu ya COVID-19.**

covidrentrelief.alleghenycounty.us

Jinsi mchakato wa maombi unavyofanya kazi



1.

Maombi yanapatikana tu mtandaoni. Ikiwa huwezi kuwa mtandaoni au unahitaji msaada ili uweze kuyajaza, piga simu ACTION-Housing kupitia 412-248-0021 au rentalassistance@actionhousing.org. Vituo vya kufikia vyenye WiFi ya bure na kmpyuta pia vitakuwa wazi katika kaunti yote. Baadhi ya vituo hivyo vina skana na wafanyakazi kwa ajili ya kusaidia kutumia teknolojia.



2.

Unapaswa kutengeneza jina la mtumiaji na nenosiri ili uweze kufikia maombi hayo. Ili ufanye hivyo, utahitaji kuwa na barua pepe. Huna barua pepe? Jisajili bila malipo kupitia bit.ly/gmailforrent au bit.ly/yahoorrent.



3.

Andika jina lako la mtumiaji na nenosiri mahali ambapo unaweza kuliona. Utalihitaji ikiwa utarudi kwenye maombi ili uweke hati, kubadilisha maelezo ya mawasiliano yako au kuangalia hali ya maombi yako.



4.

Baada ya kuwa umewasilisha maombi yako, yatapitia hatua tano:

- Tathmini ya Maombi
- Kuwasiliana na Mpangaji - Mtu atawasiliana na wewe ikiwa maelezo zaidi yanahitajika.
- Kuamua Ustahili - Ikiwa utakidhi vigezo vya ustahili, maombi yako yatahamia hatua inayofuata. Ikiwa sivyo, utapokea taarifa ya kukataliwa katika maandishi ambayo unaweza kuikatia rufaa.
- Kuwasiliana na Mwenye Nyumba
- Uchakataji wa Malipo



Unaweza kuona maombi yako yamefika wapi katika mchakato huu wakati wowote kwa kuingia tena kwenye akaunti.



5.

Tutawasiliana na wewe kuhusu kile kinachofuatia. Mtu ambaye atawasiliana na wewe anaweza kuwa anatoka ACTION-Housing, The Urban League tawi la Greater Pittsburgh au YWCA tawi la Greater Pittsburgh. Sote tunafanya kazi pamoja kwa hivyo pokea simu zao au jibu barua pepe zao.



**Una maswali? Wasiliana na ACTION-Housing kupitia
412-248-0021 au rentalassistance@actionhousing.org.**